

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA.

### MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI TAREHE 02.11.2021.

#### MAHUDHURIO:

NA.	JINA	CHEO	WADHIFA
1.	Martin Y. Mahinda	DEO	Mwenyekiti
2.	Steward Eliack	HPMU	Katibu
3.	Flora S.Malima	DHRO	Mjumbe
4.	Lucas Mirambo	DAICO	Mjumbe
5.	Simeon Twiyogoye	LFO	Mjumbe
6.	Theogonius E. Ligonja	DCDO	Mjumbe

#### SEKRETARIETI:

NA.	JINA
1.	Catherine John

#### AGENDA ZA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI

Katibu aliwasilisha agenda za kikao ambapo agenda zote zilipokelewa kama ifuatavyo:

1. Kufungua kikao.
2. Kupitia na kuridhia muhtasari wa bodi ya zabuni wa tarehe 28/10/2022
3. Mapendekezo ya kutumia Force Account kwenye ujenzi wa mradi wa UVIKO 19 Mradi No. 5441-TCRP kwa fedha za IMF
4. Kuridhia ununuzi wa vifaa vya miradi ya UVIKO-19
5. Mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti.
6. Kufunga Kikao.

#### MUHT.NA.BYZ/2021/2022/01. KUFUNGUA KIKAO.

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao akiwasisitiza kupitia agenda kwa umakini na kujadili na hatimaye kutoa maamuzi sahihi. Baada ya kusema hayo akafungua kikao mnamo saa 05:00 Asubuhi.

#### MUHT.NA. BYZ/2021/2022/02: KUPITIA NA KURIDHIA MUHTASARI WA BODI YA ZABUNI WA TAREHE 28/10/2022

Katibu aliwasomea wajumbe muhtasari wa kikao kilichopita na baada ya hapo wajumbe waliridhia na kusaini

#### MUHT.NA. BYZ/2021/2022/03: MAPENDEKEZO YA KUTUMIA FORCE ACCOUNT KWENYE UJENZI WA MRADI WA UVIKO 19 MRADI No. 5441-TCRP KWA FEDHA ZA IMF

Katibu aliwasilisha mapendekezo ya kutumia njia ya Force Account kwenye utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa UVIKO 19. Wajumbe walijadili utekelezaji wa mradi huo na kwa kuwa fedha zinapelekwa kwa kila shule husika ilionekana kwamba kutumia njia ya

force Account katika kutekeleza miradi hiyo itarahisisha kukamilisha miradi kwa wakati.

#### **Maamuzi ya Bodi ya Zabuni**

Wajumbe wa bodi ya zabuni waliridhia njia ya Force Account itumike katika kutekeleza miradi ya UVIKO 19 wenye thamini ya Tsh 3,700,000,000/= (bilioni tatu na milioni mia saba tu.) na kusisitiza sheria kanuni na miongozo ya manunuzi ya umma kufuatwa katika utekelezaji.

#### **MUHT.NA. BYZ/2021/2022/04: KURIDHIA UNUNUZI WA VIFAA VYA MIRADI YA UVIKO.**

Katibu aliwasilisha ununuzi wa vifaa vya ujenzi vya miradi ya UVIKO-19 vinavyohitajika kwa haraka kutoka kwa mzabuni wa Mwanza wa Kampuni ya V.H SHAH ili ituuzie vifaa vya ujenzi kama ifutavyo;

Na.	Aina ya Vifaa	Kipimio	Idadi	Bei ya kifaa	Jumla
1.	Saruji 42.5	Bags	15,828	19,875	314,581,500.00
2.	Nondo 12mm	Pcs	1,980	26,500	52,470,000.00
3.	Nondo 8mm	Pcs	1,998	12,500	24,975,000.00
4.	Squire pipe 1x1	Pcs	2,475	14,000	34,650,000.00
<b>Jumla kuu Tshs inclusive VAT</b>					<b>426,676,500.00</b>

Hivyo basi wajumbe wa bodi ya zabuni naomba waridhie manunuzi haya ili utekelezaji wa miradi ya UVIKO-19 ya elimu Msingi na Sekondari itekelezwe kwasababu mzabuni aliyepatikana anatuuzia vifaa hivi kwa bei ya chini tofauti na wazabuni wengine na pia bei ya soko imeonekana kuwa juu zaidi ila yeye amekubali kutuuzia kwa bei ya chini.

#### **Maamuzi ya Bodi ya Zabuni**

Wajumbe wa Bodi ya zabuni walijadili na waliridhia Manunuzi hayo yafanyike kwa Mzabuni V.H. SHAH ili kwendana na muda wa miradi hiyo ya elimu Msingi na Sekondari na kusisitiza kuwa umakini uwepo pindi manunuzi hayo yanapo fanyika kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za manunuzi ya umma.


#### **MUHT.NA.BYZ/2020/2021/05: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**


Hapakuwa na mengineyo yaliyojadiliwa.

#### **MUHT.NA.BYZ/2020/2021/06: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 06.10 Mchana kwa kuwashukuru wajumbe kuweza kuhudhuria katika kikao hicho.

#### **UMETHIBITISHWA**

  
Martin Y Mahinda  
MWENYEKITI  
TAREHE: 02/11/2021

  
Steward Eliack  
KATIBU  
TAREHE: 02/11/2021